

HABARI ZA DUNIA

DUNIA ILIYO TAYARI KWA MTU

Dunia inazidi kuharibika siku hata siku. Ugaidi, vita , fujo, umaskini, njaa, kuporomoka kwa maadili, wizi, uuaji, na kudhalilisha watoto ndiyo yanaoongoza katika vichwa vha habari katika magazeti na luninga kila siku.

Kwa hali halisi sasa, dunia inaelekea katika uharibifu mkubwa, wakati watu wengine wanangoja kwa hofu kuanguka kwake, wengine wanaendelea kuishi kana kwamba hakuna kitakachotokea. Wengi wanamngoja “mtu” ambaye ana suluhisho la matatizo mengi yaliyopo duniani. Ilisemekana, “Tupe mtu mwenye majibu, hata kama ni shetani”

Biblia inasema huyo mtu anakuja. (Anaweza kuwa huko hai leo!). Atawadanganya wengi kwa nguvu zake na miujiza yake. Atakuwa na kitu ambacho kitaonekana kama suluhisho na matatizo ya dunia. Kwa muda mfupi tu, watu watalia, “Amani na usalama”, na ghafla wataona uharibifu. (1Thes. 5:3; Ufu. 8 &9).

Mpinga Kristo atajiinua mwenyewe na kujifaninisha na Mungu na atadai kuheshimiwa na kila mtu. Watakaokataa, watauwawa. Idadi kubwa wa watu waishio katika nchi watakufa.

Katika maandalizi ya kuja kwa Mtu wa Mungu, Yesu Kristo, kutawala na kumiliki dunia katika haki. (Ufu. 11:15), Mungu atamwaga hukumu juu ya hukumu katika nchi hii, na kasha Kristo atakuja tena katika utukufu mkuu na kwa neno la kinywa chake ataziharibu umoja wa nguvu wa kijeshi wa dunia hii katika eneo liljulikanalo kama Har-Magedoni. (Ufu 16:16; 19:19). Wasioamini wote watatwaliwa kutoka dunia hii kwa kuhumu na kukutana na hukumu ya mwisho kwa dhambi zao katika Kiti Cheupe cha Hukumu. (Ufu. 20:11-15).

Kristo atanzisha ufalme wake hapa duniani na kutawala

kwa haki. (Ufu. 11:15). Kutakuwa na amani ya kweli, na haki itatakuwepo kwa uhakika. Silaha za vita zitabadilishwa na kuwa vifaa vya kilimo kwa sababu ardhi ya dunia itazalisha kwa kiwango kikubwa mno na njaa haitakuwepo. Hata jangwa litastawi, Yesu Kristo, aliyewahi kukataliwa na dunia hii, atatambuliwa kuwa yeye ni Mwana wa Mungu kweli, na Mfalme wa wafalme na Bwana wa mabwana. (Luka 24:24-27; Ufu. 19:16).

Swali linalokubabili ni hili, “Je, utamkubali Yesu Kristo kabla hajarudi kuhamisha kanisa lake kutoka duniani, na “mtu” aliyepewa nguvu na shetani kudhihirishwa? (Ufu. 13:1-18). Au utaendelea kumkataa, na labda kuishi mpaka utakapokutana na hukumu ya kutisha ya dunia hii, na kwa uhakika ukutane na hukumu ya Kristo kwa ajili ya dhambi zako? (Ufu. 20:11-15).

Biblia inatuambia jinsi ambavyo tunaweza kuokolewa, si kwa hukumu ya dunia hii inayokuja, lakini kutoka katika hukumu ya milele kwa dhambi zetu vilevile. Soma injili ya Yohana uone jinsi ya kuokoka kutoka katika dhambi zako na hukumu ijayo. Hapa ni mistari michache kutoka injili ya Yohana.

“Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe wa pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele” (Yoh. 3:16).

“Amin amin nawaambia (Kristo), yeye alisikiaye neno langu na kumwamini yeye aliyenipeleka yu na uzima wa milele, wala haingii hukumuni, bali amepita kutoka mautini kuingia uzimani”. (Yoh. 5:24).

“Yesu akamwambia, mimi ndimi njia na kweli na uzima, mtu haji kwa Baba ila kwa njia ya mimi”. (Yon. 14:6).

Spread the Word

P.O. Box 7046

York, PA 17404.